



Cour
Pénale
Internationale

International
Criminal
Court

ICC-PIDS-FS-01-005/16_Swa

Licho ya mbio mbio ku Mahakama ya Kimataifa ya Jinai



Picha: Simon Bosch

Mahakama ya Kimataifa ya Jinai, inaongozwa na Mkataba wa Roma na njo tribinale ya lote ya kwanza mu dunia na yenye iliundwaka kufuatana na Makubaliano ya kimataifa juu ya kupatia malipizi batu benye balifanya maenfraksyo za kabambi sana zenye zinagusa dunia yote. Mahakama ya Kimataifa ya Jinai iliundwa na mainchi, iko na uhuru na haiko ya Umoja wa Mataifa. Makao yake makuu iko pale La Haye mu inchi ya Holande. Hata kama Nchi zinazounda Mahakama chini ya Mkataba wa Roma njo zinalipaka kazi zake, ile Mahakama inapataka vilevile misaada ya inchi, ya makundi za mainchi, ya batu, ya masosiete (entreprises) na ya bikundi bingine. Dunia yote ilikuwaka inapenda kukuwe tribinale ya kimataifa na ya lote na sasa hii wakati (XXe siècle) kumepatikana masikilizano juu ya kusema nini njo banaitaka mauaji ya kimbari, jinai dhidi ya ubinadamu na jinai za kivita. Mu masambo yenye ilifanyikaka Nuremberg na Tokyo ni benye balifanyika jinai za kivita, jinai dhidi ya amani na jinai dhidi ya ubinadamu mu vita ya pili ya dunia njo balisambishwaka. Mu miaka ya 1990 na kuendelea, kisha vita ya baridi, tribinale sawa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Yugoslavia ya zamani na ya Rwanda ziliundwaka kutokana na vile batu bote baliitika kusikuwe mufanya makosa mwenye atabakia bila kupata malipizi. Lakini, kisha kuona kama zile tribinale ziliundwaka juu ya kuangalia tu maenfraksyo za kabambi zenye zilifanyikaka mu wakati na mu vita fulani, kulikuwa lazima zaidi ya kuunda tribinale ya kimataifa ya kusambisha maenfraksyo za kabambi na yenye iko na uhuru tena ya lote. Siku 17 ya mwezi wa saba 1998, dunia yote ilifanya neno mkubwa wakati inchi 120 ziliitika Mkataba wa Roma yenye inaunda, kufuatana na sheria, Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya lote. Mkataba wa Roma ilianza kutumika siku 1 ya mwezi wa saba 2002, kisha kutiliwa saina na inchi 60.

Uwezo wa kisheria

Mahakama ya kimataifa ya Jinai inaweza kusambisha maneno yenye inaangalia maenfraksyo za kabambi zenye zinagusa dunia yote, njo kusema, mauaji ya kimbari, jinai

dhidi ya ubinadmu na jinai za kivita, kama zilifanyika kisha siku 1 ya mwezi wa saba 2002. Mkataba wa Roma na kartasi zingine za lazima za sheria zinasema ile maenfraksyo za kabambi njo nini. Mahakama itaweza kusambisha maneno yenye inaangalia jinai ya uvamizi wakati Baraza la Nchi zinazounda Mahakama itasema jinai ya uvamizi njo nini. Mahakama itaweza tu kusambisha maneno yenye inaangalia ile maenfraksyo za kabambi kama zilifanyika mu Nchi zinazounda Mahakama wala zilifanyiwa na mutu wa muzile mainchi. Lakini haiko lazima kuheshimia hii mipaka kama Baraza la Usalama ya Umoja wa Mataifa, yenye masemi yake inapashwa kuheshimiwa na mainchi zote za Umoja wa Mataifa, njo imebeba hali kwa Prokirere, wala kama inchi moya inasema aseme inaitika uwezo wa kisheria ya Mahakama.

Kazi ya Mahakama ni kusaidia, apana kukamata fasi ya tribinale za mumainchi. Inaweza kusambisha batu kama tu tribinale za mumainchi hazisambishe bale batu wala kama zinasema aseme zitabasambisha na kisha hazipendi wala hazina namuna ya kubasambisha muzuri. Hii kanuni ya lazima njo banaitaka kanuni ya kusaidiana sababu Mahakama haina namuna ya kusambisha batu bote benyi balifanya maenfraksyo za kabambi zenye zinagusa dunia yote. Tena nia ya Mahakama ni kufikisha mbele ya sheria batu bote benye banabeba muzigo mkubwa ya maenfraksyo za kabambi zenye zinagusa dunia yote.

Kuko namuna tatu zenye Prokirere anaweza kutumia juu ya kufanya ankete wala kushtaki batu :

- Nchi zinazounda Mahakama zinaweza kufikisha hali kwa Prokirere;
- Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa inaweza kuomba Prokirere aanze ankete;
- Prokirere anaweza kuanza ankete proprio motu (ku nia yake yepeke) kufuatana na habari za kuaminika zenye alipata. Mbele ya kufanya vile, Prokirere anapashwa kuomba ruhusa ya Chumba cha utangulizi yenye inaundwa na bajije tatu benye bako huru.

Kutokuwa yulu ya sheria

Kuwa prezida, ministre wala depite, wala mutu mwenye balichagua ku buchaguzi wala mufanyakazi wa leta haiwezi kuacha mutu asisambishwe wala kupewa malipizi ya makosa yake. Bakubwa ya kazi wala bakubwa ya kisoda banaweza kubeba mzigo ya makosa yenye batu ba chini yabo benye banaongozwa nabo balifanya. Lakini Mahakama ya Kimataifa ya Jinai haiwezi kusambisha batu benye balikuwa na miaka chini ya 18 wakati enfraksyo ya kabambi yenye inasemekana inaweza kuwa ilifanyikaka.

Haki za baviiktime na za benye kushtakiwa

Kufuatana na kanuni zenye zinaongoza Mahakama ya Kimataifa ya Jinai, baviiktime banaweza kutumia Prokirere habari juu ya maenfraksyo za kabambi zenye Mahakama iko na uwezo ya kusambisha. Njo turu ya kwanza, mu historia ya sheria ya kimataifa, baviiktime kupewa haki ya kuwa na neno mu masambo na ya kuomba malipo. Nikusema banaweza kuya ile fasi ya kusambishia sawa vile batemwe na banaweza kueleza mawazo na shida zabo mu kila kipindi ya masambo. Juu ya ile, bako na mwenye anaweza kubasimamia mbele ya sheria na kama ni lazima, banaweza kupewa msaada ya kisheria.

Biro ya Grefye inasaidiaka baviiktime na batemwe mu kupigania haki zabo, na inabapatiaka msaada ile wakati yote ya masambo na kama ni lazima, inabachungaka. Mahakama inaweza kuamua namuna mbali mbali za malipo juu ya baviiktime ; ni sawa vile kubarudishia bitu byabo, kubarudishia heshima na kubalipa franka.

Nchi zinazounda Mahakama chini ya Mkataba wa Roma ziko na Mfuko wa Dhamana juu ya baviiktime ba maenfraksyo za kabambi zenye Mahakama iko na uwezo ya kusambisha na majamaa zabo juu ya kuwezesha namuna fulani ya malipo hata kama mwenye amehukumiwa hana mali ya kutosha juu ya kulipa.

Kuchunga haki za mwenye kushtakiwa ni ya lazima juu ya masambo ya haki na sheria ya muzuri. Biro ya Grefye inaangaliaka shida za mwenye anashtakiwa ; ilifanyika liste ya majina ya baavoka juu ijuwe kama, kufuatana na Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, baavoka benye batasamba ku Mahakama banajuwa kazi na kama banaheshimia kanuni za ginsi banapashwa kujikamata wakati yote ya masambo. Mahakama inapatia bikundi bya baavoka msaada ya bitu na fasi na kama ni lazima, msaada ya franka.

Ginsi Mahakama inaundwa

Biro ya Prezida

Mu Biro ya Prezida muko Prezida Bw. Sang-Hyun Song (Korea), na bamakamu ba prezida, Bi. jije Fatoumata Dembele Diarra (Mali), makamu wa kwanza wa prezida, na Bw. jije Hans-Peter Kaul (Ujerumani), makamu wa pili wa prezida, balichaguliwaka mu bajije 18 ba Mahakama ya Kimataifa ya Jinai. Biro ya Prezida iko na kazi ya kuongoza muzuri Mahakama yote, kuacha tu Biro ya Prokirere. Inafanyika kazi pamoya na Biro ya Prokirere na inaiombaka shauri ku byenye binaangalia mafaa ya bote. Mu kazi za Biro ya Prezida muko zimoya zenye zinaangaliana na kusambisha na maongezi na batu wala makundi ya inje.

Matawi

Matawi zote tatu za Mahakama, nikusema Tawi la utangulizi, Tawi la kesi, na Tawi la rufaa, ziko ndani bajije 18. Bajije ni batu benye banaheshimiwa sana na ni batu benye banajulikana juu ya usawa yabo ; banachaguliwaka na Nchi zinazounda Mahakama mu batu kutoka dunia mzima kufuatana na ginsi banajua mzuri sheria ya makosa na utaratibu wa jinai ao mu maneno ya lazima ya sheria ya kimataifa sawa vile sheria ya kimataifa yenye inaangaliana na vita na haki za binadamu. Bajije banafanyika yote kusudi masambo ikuwe ya haki na ipitike mu hali muzuri.

Biro ya Prokirere

Biro ya Prokirere inaongozwa na Bw. Luis Moreno Ocampo wa Ajentina, mwenye anasaidiwa na makamu wa prokirere, Bi. Fatou Bensouda wa Gambia. Prokirere na makamu wa prokirere banachaguliwaka na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama. Biro ya Prokirere iko na kazi ya kupokea na kujifunza habari kusudi ya kuona kama kuko sababu za kutosha za kuanza ankete, za kufanya ankete juu ya matendo ya mauaji ya kimbari, jinai dhidi ya ubinadamu na jinai za kivita na, kushtaki benye balifanya zile maenfraksyo za kabambi. Biro ya Prokirere iko na uhuru mbele ya Mahakama.

Biro ya Grefye

Mkubwa wa Biro ya Grefye ni Bi. Silvana Arbia (Italia), anasaidiwa na makamu wa Grefye, Bw. Didier Preira (Senegal). Biro ya Grefye inapanaka msaada ya kimahakama na ya utawala ku vyombo vyote vya Mahakama. Inatumikaka kazi zingine zenye zinaangalia mwenye kushtakiwa, baviiktime na batemwe, kuelimisha batu na vile vile zenye kuangaliana na kufungwa. Ku byenye kuelekea kazi mbali mbali za Mahakama inje ya makao yake makuu, inashurulikaka zaidi na kupana msaada ya utawala ku Kundi za Biro ya Grefye na za Biro ya Prokirere na, inafanyika vile vile kazi zake za pekee. Kanuni ya kutokuwa na upendeleo mu hali yoyote njo inatawala kazi za Biro ya Grefye, hii ni kusudi hii biro ipane msaada wa sawa sawa ku kazi zote za Mahakama.

Baraza la Nchi zinazounda Mahakama

Baraza la Nchi zinazounda Mahakama iko na kazi ya kuangalia namuna gani Mahakama iko ina fanya kazi na inatiaka kanuni za sheria zenye Mahakama itatumikisha. Iko ndani benye banasimamia mainchi zenye zilitiaka saina Mkataba wa Roma wala kuiitika. Baraza la Nchi zinazounda Mahakama iko na biro mwenye muko : Prezida, ba makamu ba prezida bawili na banamemba 18 benye banachaguliwaka na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama kwa muda ya miaka 3 kwa ginsi kukuwe batu ba ngambo zote za mu dunia na ba mu namuna zote za mkubwa za sheria za mu dunia. Baraza la Nchi zinazounda Mahakama iko na biro ya sekrete ya lote kule La Haye, ku makao makuu ya Mahakama. Ile Baraza inakamata mipango yenye inaangalia shida mbalimbali, sawa vile kupitisha sheria na bajeti, na tena kuchagua bajije, Prokirere na bamakamu ba prokirere .